

Somo la 1: Kujiandaa kwa ajili ya, na kuongoza mikutano

Unaweza kufundisha somo hili lote katika ujumla wake au ukaligawa katika sehemu fupi fupi. Tohoa somo kulingana na hali ya eneo lako na mahitaji, umri, na uelewa wa urais wako wa akidi au wa darasa.

BWANA ANATUALIKA KUJIANDAA WENYEWWE

Soma [Mafundisho na Maagano 88:119](#). Jadilianeni jinsi maelekezo ya Bwana “jiandaeni wenyewe” yanavyotumika kwenye mikutano ya urais wa akidi na wa darasa. Je, ni mambo gani ambayo tunaweza kufanya ili kuandaa mikutano yetu?

KUPANGA KWA AJILI YA MIKUTANO KUNATUSAIDIA KUPANGA KAZI YA BWANA

Saidia urais wa akidi au wa darasa kujaza [mfano wa ajenda](#) katika matayarisho kwa ajili ya mkutano wao ujao wa urais. Fikiria kujadiliana pamoja maswali yafuatayo:

- Je, kwa nini ni muhimu kuzingatia maswali kama hayo kwenye mfano wa ajenda?
- Mikutano gani mingine au shughuli tungeweza kujiandaa kwazo kwa njia hii?
- Ni kwa jinsi gani tunaweza kumwalika Roho Mtakatifu kutusaidia tunapopanga na kuongoza mikutano? (Ona [Moroni 6:9](#); [Mafundisho na Maagano 46:2](#).)

Ungeweza pia kuwaalika washiriki wa urais kuandaa ajenda kwa ajili ya mkutano ujao wa akidi au darasa ambao unafuata muhtasari uliotolewa katika kila somo kwenye [Njoo, Unifuata—Kwa ajili ya Akidi za Ukuhani wa Haruni na madarasa ya Wasichana](#). Waalike kufikiri kuhusu vipengele walivyojadiliana katika mkutano wao wa urais ambavyo pia vinahitaji kujadiliwa na washiriki wa akidi na darasa. Kama muda unaruhusu, ungeweza kuwaalika kufanya majaribio ya kuongoza mkutano kwa kutumia ajenda waliyotayarisha.

Kila baada ya muda fulani, unaweza kutaka kujadili jinsi washiriki wa urais walivyohisi kuhusu mkutano. Kama sehemu ya majadiliano haya, Ungeweza kuuliza maswali kama yafuatayo:

- Je, mkutano ulikamilisha kile tulicho kusudia?
- Tulifanya nini kumwalika Roho katika mkutano? (Ona [Mafundisho na Maagano 6:32](#).)
- Je, tulijaribu kumhusisha kila mtu?
- Jinsi gani tunaweza kuboresha?

NYENZO SAIDIZI

- *General Handbook: Serving in The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints*, 10.4, 11.3.4, ChurchofJesusChrist.org